# CLASS 8 MID TERM 2 2020

# KISWAHILI

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 hadi 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa kujaza nafasi.***

Mjomba ___1___ Shauriyako alichapa kazi ya ___2___ kule ___3___. Alisifika ___4___ ___5___ wake wa ___6___ samaki wakubwa wakubwa. Siku moja aliwanasa ___7___ ___8___ wakubwa ajabu. Baada ya kuuza ___9___ lake aliwalipia watoto wake ___10___ shuleni.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. yake | B. zao | C. zake | D. wake |
| **2.** | A. ukulima | B. ualimu | C. uvuvi | D. utopasi |
| **3.** | A. bahari | B. baharini | C. mto | D. ziwa |
| **4.** | A. kwa | B. na | C. soma | D. sifa |
| **5.** | A. hodari | B. uhodari | C. mbio | D. haraka |
| **6.** | A. kumnasa | B. kupata | C. kuuwa | D. kuwanasa |
| **7.** | A. wakunga | B. makunga | C. mikunga | D. dagaa |
| **8.** | A. watisa | B. tano | C. tatu | D. wanne |
| **9.** | A. windo | B. mawindo | C. samaki | D. mali |
| **10.** | A. nauli | B. fola | C. karo | D. ushuru |

Mitaa ya ___11___ inaendelea kupanuka kila ___12___. Jambo ___13___ linachangiwa pakubwa na kiwango cha umaskini ___14___ kukita mizizi ___15___ na ukosefu wa ajira.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **11.** | A. kijiji | B. mabandani | C. kifahari | D. mabanda |
| **12.** | A. usiku | B. mwaka | C. uchao | D. mara |
| **13.** | A. ili | B. hili | C. hilo | D. haya |
| **14.** | A. kinachoendelea | B. unaoendelea | C. kilichoendelea | D. utakaoendelea |
| **15.** | A. pasipo | B. pamoja | C. pia | D. tena |

***Kutoka swali la 16 hadi 30, chagua jibu sahihi kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16.** Mheshimiwa, nana, hayati, bwana - maneno haya kwa jumla yanaitwa

A. adabu B. heshima

C. nemsi D. salamu

**17.** Chagua umoja wa sentensi ifuatayo;
Madobi wanaosimama karibu na kuta wana nyuta

A. Dobi anaosimama karibu na ukuta ana uta

B. Dobi anayesimama karibu na ukuta ana uta

C. Madobi anayesimama karibu na kuta ana uta

D. Dobi anayesimama karibu na nyuta ana uta

**18.** Jibu la **"makiwa"** ni **"tunayo"** au pia laweza kuwa

A. yamepita B. asante

C. nashukuru D. inshallah

**19.** Chagua maelezo ambayo si sahihi;

A. Mwiku ni chakula kilicholala

B. Makombo ni chakula kilichobaki baada ya kula

C. Kukauza ni kupasha chakula moto

D. Kilalio ni chakula cha asubuhi

**20.** Ni sentensi gani inayoonyesha **"<u>Ni</u>"** ya wingi.

A. Yeye ni mwerevu kuliko wote

B. Kitabu kimo mezani

C. Someni kwa bidii mpite mtihani

D. Alipoenda ulaya alinisaidia kulipa karo

**21.** **O-** tamati katika sentensi ifuatayo itakuwa "Watoto ambao wanacheza mtoni wataadhibiwa"

A. Watoto wanaocheza mtoni wataadhibiwa

B. Watoto wachezao mtoni wataadhibiwa

C. Mtoto ambaye anacheza mtoni ataadhibiwa

D. Mtoto achezaye mtoni ataadhibiwa

**22.** Chagua neno lenye maana ya **<u>pasipo</u>**

A. mighairi

B. mathalani

C. ilhali

D. seuze

**23.** Chagua methali ambayo haiambatani na maelezo yafuatayo;
Iwapo mtu anataka kufaidika kutokana na kazi yake, sharti kuwa tayari kufanya kazi.

A. Atangaye sana na jua hujua

B. Penye mawimbi na milango i papo

C. Achanikaye kwenye mpini hafi njaa

D. Anayetafuta hachoki, akichoka keshapata

**24.** Taibu! Shabash! Kefle! Po! yote ni

A. viwakilishi B. vielezi

C. vihusishi D. vihisishi

**25.** Kitenzi cha kurudisha mwanga uliopiga kwenye kioo ni

A. ajizi B. akisi

C. mwangwi D. mwangaza

**26.** Chagua kiambishi mwafaka kujaza pengo
Chatu haku__________nasa swala.

A. m B. i

C. li D. ki

**27.** Kazibovu alipotembelea kituo cha afya kujua hali yake alifahamishwa na daktari kuwa yeye ni H.I.V chanya - maana yake ni

A. Kazibovu ana virusi vya ukimwi

B. Kazibovu hawezi kupata virusi vya ukimwi

C. Kazibovu ni mgonjwa

D. Kazibovu hana virusi vya ukimwi

**28.** Tegua kitendawili;
Anafahamu kuchora lakini hajui achoracho.

A. Mtoto B. Konokono

C. Tingatinga D. Kalamu

**29.** Chagua sentensi yenye kielezi cha wakati

A. Mtoto alitembea kimnyonge

B. Baada ya ibada nitasafiri

C. Waliabiri gari la mwalimu

D. Mzembe huchelewa kila mara

**30.** Stadi wa kufunga mashairi ni malenga, naye stadi wa kupiga ngoma ni

A. manju B. ghariba

C. sogora D. mkwiro

***Soma kifungu kwa makini kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***

Usafiri kwa bodaboda umekuwa mashuhuri sana nchini mwetu. Siamini kama sasa ipo sehemu yoyote nchini mwetu ambako hakuna bodaboda. Sababu kuu ni kuwa serikali ilipunguza ushuru unaotozwa pikipiki zinazoletwa nchini kutoka ughaibuni. Hivyo bei yake ikashuka.

Sina shaka wala tashwishi kuwa pikipiki hizi zimewafungulia vijana wengi ajira. Familia kadhaa zimepata mkate wao wa kila siku. Usafiri mashambani umerahisishwa. Wateja ni wengi. Vijana waliokuwa na tabia ya kurandaranda kama mbwakoko sasa wamepata shughuli ya kuwaletea mapato. Wengi waliotekwa nyara na mvinyo na vileo sasa wana kila sababu ya kutabasamu. Visa vya uhuni vimepungua.

Ni kweli kuwa hakuna masika yasiyokuwa na mbu. Licha ya manufaa haya, bodaboda zimekuwa chanzo cha madhila kadhaa. Cha mno ni kuwa waja wengi wametutangulia mbele ya haki baada ya kuhusika katika ajali zinazohusisha bodaboda.

Ni kosa mbaya kwa mwendeshaji wa chombo hiki chenye magurudumu mawili kuwasiliana kwa rununu akikiendesha. Iwapo atashindwa kukidhibiti ole wenu mnaoabiri!

Nimeshuhudia si mara moja ikiwabeba wateja zaidi ya wanne. Si huku ni kusaka tikiti ya kwenda kwa muumba wako? Tamaa ya fedha ndiyo chanzo cha haya yote. Iwapo ajali itatokea huenda wateja wakapata majeraha mabaya hata kuvunjikavunjika.

Ubebaji wa mafurushi makubwa kupita kiasi umechangia pia. Wapo waendeshaji wa bodaboda ambao hupuuza hadharani sheria za barabarani hasa mijini. Baadhi yao hupitia vinjia ambavyo vimejengwa na kutengewa wasafiri wa **kupiga miludi**. Wamewagonga watembeaji wasiokuwa na hatia na hasa wengine kupata tikiti ya kwenda katika dunia isiyo na marejeo.

Ni kosa kubeba zaidi ya mteja mmoja. Ni jambo la busara kuvalia ile kofia maalum ya pikipiki ili kujikinga na majeraha hasa ya kichwa iwapo ajali itatokea.

Tamati, ninawashtumu baadhi ya waendeshaji bodaboda ambao wamekuwa wachafu afadhali fuko. Wananuka makwapani. Kupiga mswaki wamesahau kabisa. Wao hunuka kimenomeno. Pongezi kwenu mnaozingatia usafi wa miili yenu na mavazi yenu!

**31.** Ni kauli gani ambayo sio sahihi kulingana na aya ya kwanza?
A. Bodaboda ni mashuhuri sana
B. Pikipiki huagizwa kutoka ng'ambo
C. Ushuru wa pikipiki umepunguzwa
D. Bei ya pikipiki imepanda

**32.** Katika aya ya pili mwandishi hasemi kuwa
A. pikipiki zimefungua nafasi za ajira
B. usafiri mashambani sasa ni rahisi
C. vijana sasa ni walevi kule mashambani
D. familia zimepata mkate wa kila siku

**33.** Ni yapi ambayo ni manufaa ya bodaboda kwa vijana
A. Ulevi B. Ajira
C. Kuzurura D. Ajali

**34.** Kulingana na kifungu, ni jambo gani ambalo haliafikiani na haya mengine?
A. Riziki katika familia B. Majeraha mabaya
C. Kupoteza maisha D. Waja kuvunjikavunjika

**35.** Kulingana na mwandishi, ni kosa gani ambalo mwendeshaji bodaboda anaweza kufanya akiiendesha pikipiki?
A. Kuwabeba wateja wengi
B. Kuyabeba mafurushi makubwa
C. Kuwasiliana kwa rununu
D. Kuwa mchafu

**36.** Ni tukio gani ambalo huonyesha hadhara ukosefu wa nidhamu kwa waendeshaji bodaboda?
A. Kufuata sheria
B. Kutofuata sheria
C. Kuwabeba wateja hata zaidi ya wanne
D. Kupitia vinjia vilivyojengewa wasafiri wa miguu

**37.** Ni jambo gani ambalo halichangii ongezeko la idadi za ajali za bodaboda?
A. Kubeba mafurushi kupita kiasi
B. Kuwasiliana kwa simu
C. Kupitia vinjia vya wasafiri wa miguu
D. Kuwabeba wateja zaidi ya mmoja

**38.** Mteja wa bodaboda anashauriwa
A. kuvalia ile kofia maalum
B. kuvalia kofia kila wakati
C. kuwa na busara
D. kujikinga

**39.** Ni nini maana ya kifungu hiki **'kupiga milundi?"**
A. Kutembea haraka
B. Kutembea polepole
C. Kutembea kwa miguu
D. Kujikokota

**40.** Ni nani ambao hawajashtumiwa na mwandishi?
A. Waendeshaji wa bodaboda wachafu
B. Wasafiri wanaotumia bodaboda
C. Waendeshaji bodaboda wasiopiga mswaki
D. Fuko

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 hadi 50.***

Siku nyingi **alilalia mate**! Umaskini na ufukara ndio uliokuwa chanzo cha masaibu yake! Licha ya hayo yote alijikaza kisabuni, naye Mola akamjalia kichwa chepesi. Huyo si mwingine bali ni Mweledi.

Kipawa cha usanii kilijitokeza tangu utotoni. Nao walimu hawakuchelewa kukitambua na kukikuza kipawa hicho nadra. Akiwa katika darasa la pili, Mweledi alikuwa stadi wa kughani mashairi aina ya tarbia. Uigizaji wake ulikuwa na ubunifu wa juu usiokuwa wa kiwango chake.

Wengi walivutiwa na sauti yake ya ninga. Shuleni aliwatumbuiza wenzake zaidi ya mia sita. Hadhira yake haikukosa walimu na hata wazazi. Kila juma alighani shairi moja, naye akawa wa kuigwa na wengi. Hakuna mmoja aliyetamani kukosa shule siku ya Alhamisi siku ya shairi.

Kipawa chake kilianza kufunika umaskini polepole kama kivuli! Mwalimu Chaurembo ndiye aliyejitwika jukumu la kumwongoza Mweledi. Mashairi yake yalikuwa mahususi na hayakukosa shabaha lake; si burudani, si ufisadi, si ajira na dhuluma dhidi ya watoto. Mweledi aligonga ndipo kwa usanii!

Ushujaa wake ulijitokeza bayana wakati wa sherehe za mashujaa.

Shairi lake lenye kichwa 'Ufisadi ni Saratani" liliwaacha wengi vinywa wazi. Mweledi, mtoto wa darasa la pili ajibwaga jukwaani mbele ya viongozi wakuu wa kaunti. Utulivu ulikuwa ni wa ajabu kisha sauti ya ninga ikapasua hewa.

Ubeti wa kwanza, wa pili, kabla ya kibwagizo cha ubeti wa tatu baadhi ya viongozi walianza kulengwalengwa na machozi - labda walikuwa washiriki wa uovu huo - sina habari lakini ukweli ni kuwa palipo na moshi hapakosi .......... Baada ya sherehe gavana wake alimtuza hela kadhaa.

Upeo wa usanii wake ulikuwa ni wakati wa mkutano wa hadhara uliohutubiwa na mheshimiwa rais. Shairi lake liligusa hisia na nafsi za kila aliyekuwepo. Hapo alipata ufadhili wa masomo nao wavyele wake wakajengewa nyumba nzuri. Umaskini ukazikwa katika kaburi la sahau.

**41.** Chanzo cha shida za Mweledi kilikuwa ni
A. kulalia mate B. Mola
C. kipawa D. umaskini

**42.** Kulingana na aya ya pili, walimu walitekeleza wajibu gani kumsaidia Mweledi?
A. Kutambua kipawa
B. Kukuza kipawa
C. Kutambua na kukuza kipawa
D. kughani mashairi

**43.** Ni ipi ambayo si sifa ya Mweledi?
A. Mbunifu B. Mcheshi
C. Mwenye Bidii D. Jasiri

**44.** Kulingana na aya ya tatu, ni kipi ambacho kilikuwa cha hadhira ya Mweledi?
A. Sauti B. Ubunifu
C. Bidii D. Ughani

**45.** Kulingana na maoni ya mwandishi, ni njia gani ambayo shule ilisaidia pakubwa kukuza kipawa cha Mweledi?
A. Kutambua kipawa
B. Kumpa nafasi
C. Kutenga siku ya kukariri shairi
D. Kuwa msanii hodari

**46.** Kulingana na kifungu, lengo la shairi la Mweledi si pamoja na
A. kuburudisha
B. kukashifu
C. kuelimisha
D. kuhubiri

**47.** Kipawa cha Mweledi kilianza kuzaa matunda wakati wa
A. siku za Alhamisi
B. sherehe za mashujaa
C. mkutano wa hadhara
D. Ijumaa

**48.** Ni wazi kuwa
A. Mweledi alifaidika na kipawa chake
B. Gavana hakupendezwa na usanii wa Mweledi
C. hakuna mafisadi walioguzwa na ujumbe wa Mweledi
D. mashairi hayakuwapendeza baadhi ya viongozi

**49.** Ni nini maana ya msemo **"lalia mate"** kama ilivyotumika katika kifungu?
A. Kula sana
B. Kulala bila chakula
C. Kuwa na ndoto za ajabu
D. Kuona shida nyingi

**50.** Upeo wa usanii wa Mweledi ulikuwa ni
A. kusaidiwa na rais
B. kughani mashairi
C. kutuzwa na gavana
D. kumaliza masomo yake